

**Rafiki Mpendwa,**

Ni matumaini yetu kuwa, kijarida hiki cha kwanza kwa mwaka 2010 kimekukuta ukiwa na afya njema, nguvu za kutosha na utayari wa kuendelea kupambana na umaskini uliokithiri. Tunatarajia kwamba kila mmoja ni mzima katika familia yenu pia.

Kwa mara nyingine tena, wiki 5 zilizopita Haiti ilikuwa ikiboreka katika kuelekea mafanikio ya baadaye kwa watu wake. Tunawajua watu wa Haiti na wanatakiwa kuwa ni mfano wa kuigwa na dunia. Ushujaa, busara na umoja wao ni imara kuliko matatizo na majanga yanayo ikumba na kuathiri nchi yao.

**Dear friend,**

We hope this 1<sup>st</sup> 2010 Newsletter finds you in good health, full of strength and willingness to continue the struggle against extreme poverty. We trust everybody is fine in your family as well.

Five weeks ago Haiti once again has been battered in its progress towards a better future for all. We know the Haitian people, and we know that they should be a guiding reference for the world. Their courage, wisdom and solidarity are stronger than the misery and catastrophes gripping their country.

**Ushujaa na Utu wa watu wa Haiti**

Kupitia magazeti, radio na televisheni, tuligundua upana wa dharuba na pia kiasi cha misaada itolewayo na nchi mbalimbali duniani. Misaada ya kimataifa ni muhimu sana na tunafurahishwa na upatikanaji huu mkubwa wa misaada. Hata hivyo, tulitambua kuwa vyombo vingi vya habari vimekuwa vikiongelea zaidi uhamasishaji huu wa utoaji wa misaada toka nchi za nje zaidi na kwa uchache juu ya uhamasishaji miongoni mwa Wahaiti wenyewe.

Ni muhimu kuwa kumbusha kuwa ni kwa vipi Wahaiti walio masikini kabisa wamechukua hatua ya kuungana pamoja na wenzao kila siku japokuwa majanga yamekuwa yakijirudia miaka mingi iliyopita.

**Courage and dignity of Haitians**

Through newspapers, radio and TV, we discovered the extent of the catastrophe, as well the extent of the help provided by many countries around the world. This international support is vital of course and we are impressed by this huge outburst of aid. However, we note that the media speak much about this mobilisation but very little about the mobilisation of the Haitians themselves.

It is essential to be reminded of how the poorest Haitians take action in solidarity with others every day, despite the repeated calamities they have undergone these past years.



*adhimisho la Oktoba 17 - Haiti - Oct. 17<sup>th</sup> celebration*



ATD Fourth World Movement - P.O. Box 61786 - Dar es Salaam  
 mail : [atd.tanzania@gmail.com](mailto:atd.tanzania@gmail.com) - tel : 022 - 276 17 17  
 English website : [www.atd-fourthworld.org/-Tanzania,549-.html](http://www.atd-fourthworld.org/-Tanzania,549-.html)  
 Tovuti ya Kiswahili : [www.atd-fourthworld.org/-Kiswahili-.html](http://www.atd-fourthworld.org/-Kiswahili-.html)

Nerline, rafiki wa ATD alisema : *"Nilikuwa nikiwatembelea watu waliobaki katika maeneo ambayo bado ni hatarishi. Ardhi ilikuwa yenye utelezi na imevurugika kila mahali. Nyumba zilibaki magofu na zimesimama bila kukamilika. Hata tulipojaribu kuwashauri kuondoka, hawakutaka kuyaacha mazingira yao. Walibaki pamoja na waliojeruhiwa na hata waliofariki pia. Walikuwa na sababu zao japokuwa kila kitu kilikuwa kimeathiriwa. Hatukujua ni kwanini, lakini kama hatukuwa tumewatembelea basi naamini hakuna hata mtu mmoja ambaye angali watembelea."*

St Jean, rafiki mwingine wa ATD aliongeza : *"Bado tupo hapa, watu wana wasiwasi na hali ya njaa kwani akiba waliyonayo inazidi kupungua. Hatujui ni vipi tutaanza maisha yetu upya, ila umoja ndio unao endesha nchi yetu. Mfumo wa kiserikali utakao endelea kutuongoza nchini petu ni wa umoja na mshikamano."*



*shughuli ya shule ya awali - Haiti - pre-school activity*

Mwandishi wa Kihaiti Dany Laferriere alisema katika mahojiano kuwa: *"Baada ya tetemeko, kilicho saidia mji huu ni nguvu za watu walio masikini kabisa. Shukrani kwao, Mji wa Port-au-Prince unaonekana."*

Kivipi tunaweza kuzuia maafa tunayoyaona katika vyombo vya habari kwa watu wa Haiti? Kivipi tunaweza kuendelea kuona hali ya umoja kwa vitendo, umoja uliojengwa na historia, kwa moyo wa kizalendo na vitendo, ushujaa, dhamira na imani ya watu wa Haiti?

*Kutokana na heshima ya watu wa Haiti, janga hili ni changamoto kutufanya kutumia njia mbadala kuweza kuchukua hatua kwa pamoja ambapo rasilimali watu pamoja na vitendea kazi vitokavyo nje ya Haiti vinaendana na changamoto zilizopo ikihusisha wataalamu, nguvu kazi, ubonifu na uzoefu wa watu wa Haiti na hasa wale wanaoishi katika mazingira duni zaidi, na umaskini uliokithiri.*

Nerline, an ATD friend said : *"I've been visiting people who remain in the zones that are still somewhat dangerous. The land is slippery everywhere. Houses are still partially standing. Even when we advise people to leave, they do not want to leave their surroundings. They stay put, with the wounded, and even with the dead. They have their reasons, even if everything is shattered. We do not know why. But if we did not visit them, no one else would."*

St Jean, another ATD friend added : *"We're still here. But people's resilience is weakening because the few provisions people had are diminishing. We do not know how life will begin again, but it is solidarity that is governing our country. The one form of government that must continue is that of the solidarity guiding our country."*

The Haitian writer Dany Laferrière said in an interview : *"After the earthquake, what saved this city was the energy of the poorest people. Thanks to them, Port-au-Prince is still alive."*

How can we avoid being submerged by a flood of images? How can we **stay attentive to the gestures of solidarity** building up from the depths of this country, its history and its soul through the hands, courage, minds and faith of its inhabitants?

*Out of respect for the Haitian people, this catastrophe must become an opportunity to **develop a new way of taking action collectively, where human and material resources coming from the outside accept the challenge of blending with the intelligence, drive, creativity, and experience of Haitians, and in particular those living in the most extreme poverty.***

## Kwa pamoja sasa na katika mipango endelevu.

Tulikuwapo Haiti tangu mwaka 1981, kundi la ATD lilianza kujihusisha na familia nyingi zilizo katika umasikini uliokithiri katika makazi tofauti tofauti. Kila siku baada ya tetemeko kikundi chetu huwatembelea familia moja baada ya nyingine, kuchukua hatua ya kurudisha malezi ya msingi na maendeleo ya watoto kama kipaumbele cha kwanza. Nia kuu ya kuwatembelea ni kuwapa nguvu ili waweze kuyakabili kwa ujumla matatizo waliyonayo kama ukosefu wa chakula, maji safi ya kunywa na huduma za afya wakati huo huo tukijaribu kuangalia ni jinsi gani tutajenga maisha bora hali yakuwa tuko katika lindi la hali ya hatari.

Walikuwa katika harakati za kuandaa mikutano pamoja na taasisi za kimataifa zenye uzoefu wa kutoa misaada mikubwa ya kibinaadamu kwa ajili ya kupata misaada zaidi, na taasisi za ndani. Lengo la ATD ni kuwezesha familia zilizotengwa kufaidika na misaada itolewayo na mitandao ya misaada.

Pia kundi la ATD limeelekeza nguvu zake katika kuanza kusafisha, kupanga na kuandaa mahala ambapo watoto watakuwa wa kikutana katika makazi ya muda. Matarajio yetu ikiwahusisha watoto na wazazi ni kushiriki miradi ya kujifunza kusoma ambayo ATD ilikuwa ikifanya na majirani zao. Shukrani kwa familia kuwa na mioyo ya ujasiri na kuwa nasi kwa muda mrefu.

Kundi lililoko Haiti, likisaidiwa na mengine ya kimataifa imeeleza malengo yake kama ifuatavyo :

- kuwa karibu na familia zifanyazo jitihada na kuziwezesha kushiriki katika kila kilicho pangwa kufanywa.
- kuwawezesha kupata huduma muhimu za kiafya.
- kushiriki katika usafi wa jiji na juhudi za urekebishaji wa miundo mbinu yake.
- kuongeza ushirikiano na watu wa Haiti na washiriki wa kimataifa ambao wanajua uwepo wao wa kujihusisha, na hakuna ambaye anaachwa nyuma.

## Together, now and in the long run

Present in Haiti since 1981, the ATD Fourth World's team created links with many extremely poor families in different neighbourhoods. Each day since the earthquake, the team visits them one by one, taking steps to resume activities promoting early childhood development as a first priority. The overall aim of these visits is to regain strength in order to collectively address the lack of food, safe drinking water and medical care, while also beginning to imagine how to build the future while still immersed in an overwhelming emergency situation.

They may also be out and about, attending meetings with the international NGOs skilled



*maktaba ya mtaa - Haiti - street library*

in large-scale humanitarian relief, or with local organisations. The team's goal remains the same: to enable families who are isolated to benefit from the help and support being put in place by aid networks.

In addition, the team started efforts to clean, prepare and organise a place in a reception camp where small children could gather. The wish of all, including parents and children, is to continue the shared-learning projects which ATD has been running in the neighbourhoods, thanks to the courage of the families, for a very long time.

The local team, supported by the International movement defined their strategies as follows :

- being close to families in their efforts to be taken into account and to be able to participate in what is being set up;
- getting access to urgent medical care;
- contributing to the city's clean up and reconstruction efforts;
- deepening the collaboration with Haitian and international partners who share the concern that no one be left behind.



Ili kuiongezea nguvu timu, kikundi cha kwanza cha watu watano, wajumbe wa muda mrefu ATD ikihusisha daktari mmoja wali ungana na kusafirishwa kwenda Haiti mwanzoni mwa mwezi Februari.

Kama marafiki wa ATD Tanzania, kwa vipi tunaweza kutoa msaada kwa ndugu zetu wa Haiti ?

- Ni muhimu sana kwa watu wa Haiti kujua kuwa popote duniani kila mmoja anafahamu ujasiri wao, ushupavu na jitihada zao. Pia ni muhimu sana kwa watu wazima kama ilivyo kwa watoto kujua kuwa wapo katika mioyo, fikra na sala zetu. Unaweza kuchora au kuandika ujumbe wa matumaini na kututumia ili kuzifikisha katika familia zinazojulikana kwa timu iliyoko Haiti.

- Zaidi ya misaada ya dharura, misaada ya muda mrefu ni muhimu sana. Marafiki wengi wamechangia fedha, iliwahusisha wale wenye kipato cha chini, wengine waliandaa shughuli za kuchangisha fedha. Tunaweza kuituma michango kwa ATD Dunia ya Nne makao makuu (usisahau kunionyesha kuwa ni mchango wako kwenda Haiti).

- Tunaweza kupata habari ya hali inayoendelea kupitia tovuti ya ATD <http://www.atd-fourthworld.org/-Haiti,329-.html> na uzisambaze habari hizi. Usisite kusoma kijarida hiki cha habari kwa ndugu zako, marafiki zako na hata majirani zako.

In order to reinforce the team, a first group of 5 long-term ATD members including a doctor was constituted and travelled to Haiti at the beginning of February.

As ATD friends in Tanzania, how can we assist our Haitian brothers ?

- It is essential for all of the Haitian people to know that everywhere in the world everybody is aware of their courage, their determination and their efforts. It is crucial for adults as well as for children to know that they are present in our hearts, our thoughts, our prayers. You can write and draw messages of hope, and address them to us so that we can pass them on to the families known by our local team in Haiti.

- Beyond the vital emergency aid, long-term support is absolutely necessary. Many friends of ATD Fourth World are already making the utmost effort to send support : some have donated money, including people who have very little to spare ; some have organised fund-raising activities. We can transfer all your donations to ATD Fourth World International Movement (don't forget to precise "Haiti" on your donation).

- We can stay informed about the situation in Haiti through the ATD website <http://www.atd-fourthworld.org/-Haiti,329-.html> and spread this information. Don't hesitate to make read this Newsletter to your relatives, your friends, your neighbours...

Wote tumeguswa sana na taabu na mshikamano wa watu wa Haiti, tunapo yaandika haya, tunafikiria majanga yaliyoko Tanzania na mahala pengine ambapo vyombo vya habari vimeweka mkazo kidogo ambapo ni maeneo yenye mafuriko, maporomoko ya udongo, kubomoka kwa migodi kama Haiti. Familia nyingi zilizoathiriwa ni zile zinazoishi katika mazingira magumu. Kwa Haiti panapotokea matukio kama haya huwalazimu kujihusisha katika kutoa misaada. Kama ulikuwa shuhuda wa hali hiyo, tafadhali tuambie.

Kuwa makini.

*Wako, Timu ya ATD Dunia ya Nne  
ya Dar es salaam.*

All of us are very touched by the suffering and the solidarity of the Haitian people. However, writing these lines, we also think about catastrophes in Tanzania and elsewhere, which the media show little interest in : landslides, floods, mines collapsing... As in Haiti, the most affected families are those who already had the hardest life. And as in Haiti, these exceptional events provoke exceptional involvements. If you were witness of such a situation, please tell us.

Take care of yourself.

*Your ATD Fourth World Team  
in Dar es Salaam*